

Mila za kukandamiza kwa jila la utamaduni

Duniani kote, viongozi wa kanisa na tamaduni wanapiga tohara ya wasichana na ndoa ya lazima.

Tohara ya wasichana inafokewa na kanisa za Kikristo, umoja wa kimataifa na imeondoolewa na sheria za Kenya lakini bado sehemu chache za jamii za Kimasaai.

Kulingana na shirika la Afya duniani, kati ya wasichana 3 na 7 kwa mia upoteza maisha baada ya kutahirishwa. Pia wengine wengi ufa kutokana na maambukizi yanayosababishwa na tohara.

Ndoa ya mapema udidimisha elimu ya msichana. Lakini shirika ambalo linaongoza kwa maendeleo ulimwenguni, Banki ya Kimataifa yasema "Uwekezaji bora duniani ni elimu ya msichana!"

„Siwezi nikaeleza machungu na bado nakumbuka vile nilivyowaza, juu ya kitendo hiki cha kuogofya na kudhulumu: Mama aliniahidi kuwa haingekuwa chungu lakini alinidanganya.“ (Nukuu kutoka kwa mwanamke aliyetahirishwa angali msichana)

Anwani

Kwa maswali na usaidizi, Tafadhali tuandikie au piga simu kwa:

Tareto Maa Organization
Pastor Daniel Ole Tiemasi

Phone number: 0729507569
P.O Box 89
Kilgoris, Kenya
Barua Pepe: contact@tareto-maa.org
Tovuti: www.tareto-maa.org

Tareto Maa ilisajiliwa kama mungaano wa kijamii mwaka wa 2009, April na wizara ya kinjisia, watoto na maendeleo za jamii.



tareto maa

**Kituo cha kuokoa watoto walio hatarini
mkoa wa transmara**



**Kupigana dhiti ya tohara ya wasichana
na ndoa ya lazima**

Tareto Maa - kusaidia wasichana walio hatarini

Lengo letu ni kuwasaidia wasichana wanaokimbia nyumbani ili kujiepusha na tohara. Tunazungumza nao, wazazi wao na kushirikiana na viongozi wa jamii ili kuwalinda.

Ikiwa hakuna suluhisho nyingine sisi huwapa wasichana hao makao mapya katika kituo chetu vilevile mayatima wasio na pa kwenda na pia kushughulikia masomo yao.

Kama shirika la kijamii sisi ni sehemu ya congregation za mitaa, The African Inland Church (AIC). AIC ni uliojengwa katika Murua / Shatuka katika Wilaya ya Transmara.

Tohara ya wasichana uwanyima haki za kibinadamu, kwa mfano:

-Kongamanbo la umoja wa kimataifa kwa haki za watoto

-Mkataba wa kiafrika kwa haki na maslahi ya mtoto

-Sheria za motto Kenya.

Watoto wana haki – mtoto msichana ana haki ya kusema "la"

Ni haki ya mtoto wa kike kusema "La" na kukataa tohara - Na ni wajibu wa mzazi kukubali kauli yake lakini wakati mwingine familia huendelea kumtisha mtoto.

Hapo ndipo Tareto Maa kama sehemu ya kanisa ya jamii ikishirikiana na kiongozi wa mkoa, wazee na wa kijiji na wasaidizi wao itaingilia kati ili kuwalinda.

Tareto Maa huwapa wasichana makao mapya yenye usalama na kuwawezesha kuenda shule pamoja na watoto wengine kwa jamii.

Tunajivunia kuwa wa Masaai – lakini mambo mengine ni lazima yabadilike

Wamasai ni warembo na ni vyema kujivunia kukuzwa kama msichana mmasai lakini kuna tamaduni zingine zimepitwa na wakati na ambazo ni za kudhumu.

Ni sababu gain ambazo wazazi hutoa? Moja ni kwamba tihara ni muhimu kwa ndoa, pili ni ishara kuwa msichana amepitia utoto na yuko tayari kuwa mwanamke na wazazi wana haja ya mahari. Lakini je hizi sababu zinadhibitisha mzazi kumdhulumu mototo kwa kumtahirisha na kumzuia kuendelea na masomo yake?

Makabila na jamii tofauti Kenya zimeonyesha kuwa tamaduni zinaweza kuboreshwa na mila kubadilishwa. Tuna haki ya kujivunia kuwa Masaai lakini tusijivune kiasi kuwa hatuwezi kusoma na kujiendelea.

